MAENDELEO BANK
Together in Progress

# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA MOJA WA MWAKA WA WANAHISA WA MAENDELEO BANK PLC

Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa Kumi na Moja wa Wanahisa wa Maendeleo Bank PLC utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 28 Juni 2025 katika ukumbi wa Msasani, Dar es Salaam kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mkutano utatanguliwa na warsha kwa Wanahisa.

## Ajenda za Mkutano ni:

1. Kufungua Mkutano
2. Kupokea na Kupitisha Ajenda za Mkutano Mkuu wa 11 wa Mwaka.
3. Kupitia na Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 10 wa Mwaka.
4. Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa 10 wa Mwaka
5. Taarifa ya Wakurugenzi kwa Mwaka Ulioishia tarehe 31 Disemba 2024
6. Taarifa ya Mkaguzi wa Nje na Taarifa za Fedha Zilizokaguliwa kwa Mwaka Ulioishia tarehe 31 Disemba 2024
7. Kupokea na Kuidhinisha mapendekezo ya Posho na Ada za Wakurugenzi kwa Mwaka 2025
8. Kupokea na Kuidhinisha Mapendekezo ya Mkaguzi wa Nje kwa Mwaka Utakaoishia Tarehe 31 Disemba 2025.
9. Kupokea na Kuidhinisha Pendekezo la Gawio.
10. Mengineyo.
11. Kupanga Tarehe ya Mkutano Mkuu wa Mwaka Ujao

## ZINGATIO:

1. Mwanahisa anayetaka kuhudhuria mkutano atajigharamia mwenyewe na anapaswa kuja kwenye mkutano akiwa na cheti cha Hisa/ Taarifa ya Akaunti inayotolewa na Soko la Hisa (DSE) na kitambulisho chenye picha kwa ajili ya utambulisho.

2. Mkutano pia utafanyika kwa njia ya mtandao wa zoom anuani ya mkutano itatumwa kwenye barua pepe au namba ya simu ya Mwanahisa iliyosajiliwa Benki. Hivyo wanahisa wanaopendelea kuhudhuria mkutano huu kwa njia ya mtandao wa zoom, wawasiliane na Katibu wa Benki kupitia barua pepe: shareholders@maendeleobank.co.tz au ujumbe wa simu / WhatsApp kupitia +255677 500050 hadi 26 Juni 2025 ili kupata taarifa na muongozo wa namna ya kushiriki kwenye mkutano huu.

3. Nakala za vitabu vya Mkutano Mkuu na fomu za uwakilishi zitapatikana Makao Makuu ya Maendeleo Bank, yaliyopo Luther House, Barabara ya Sokoine, kuanzia tarehe 19 Juni, 2025, na pia vitabu vitapatikana ukumbini hiyo tarehe 28 Juni 2025.

4. Mwanahisa anayestahili kuhudhuria Mkutano na ambaye ataona kwamba hataweza kuhudhuria yeye mwenyewe, anatakiwa kumteua Mwakilishi wake kwa kujaza fomu za uwakilishi na kuziwasilisha zikiwa zimetiwa saini na kubandikwa stempu za ushuru za TZS 500 na zifikishwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Maendeleo Bank PLC, saa 48 kabla ya tarehe ya Mkutano. Ikiwa Mwanahisa ni kampuni, fomu ya mwakilishi lazima iwe na lakiri ya kampuni na aje akiwa na cheti cha Hisa.

5. Mapendekezo yoyote ya Wanahisa yapelekwe/yatumwe kwa Katibu kupitia barua pepe **shareholders@maendeleobank.co.tz** au WhatsApp namba +255677500050 saa 48 kabla ya tarehe ya Mkutano.

KWA AGIZO LA BODI

Angela Mwageni
**Katibu wa Bodi**
**28 Mei 2025**